**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018.

Ofisi ya Bunge,
S. L. P 941,
**DODOMA**

Aprili, 2017.

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimwa Spika,** napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia uhai, afya njema na kunipa fursa ya kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine tena, napenda kumpongeza aliyekuwa Mjumbe wa Kamati hii, Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb), ambaye ameteuliwa na kupewa dhamana ya kuongoza Wizara hii muhimu ya Katiba na Sheria. Kamati inamtakia kila la heri katika kutekeleza majukumu yake mapya.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016**,** naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati ya Katiba na Sheria ina jukumu la kusimamia Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake sita (6) zifuatazo:

i. Wizara ya Katiba na Sheria **(Fungu 41)**
ii. Mwanasheria Mkuu wa Serikali **(Fungu 16)**
iii. Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka **(Fungu 35)**

iv. Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora **(Fungu 55)**

v. Tume ya Kurekebisha Sheria **(Fungu 59)**

vi. Tume ya Utumishi wa Mahakama **(Fungu 12)**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo makubwa matano yafuatayo:

(i) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016;

(ii) Utekelezaji wa mapendekezo na ushauri wa Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;

(iii) Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;

(iv) Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 pamoja na Taasisi zilizo chini yake; na

(v) Maoni na Ushauri wa Kamati.

## 2.0 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 22 Machi, 2017 Kamati ilipata fursa ya kutembelea Ofisi ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora **(Fungu 55)** zilizoko Wete - Pemba na

kupokea Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Tume kwa upande wa Pemba.

**Mheshimiwa Spika**, mpaka kufikia Machi, 2017 gharama za upangishaji na ukarabati wa jengo hili zilifikia Shilingi Milioni Arobaini (**40,000,000.00**) ambazo zimekua zikitolewa kwa awamu kuanzia Mwaka wa Fedha 2010/2011. Baada ya kufanya ziara hiyo, Kamati imeridhishwa na ukarabati na hali halisi ya mazingira ya Ofisi hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kamati kuridhishwa na hali halisi ya ukarabati na mazingira ya Ofisi hii, kuna changamoto ya kiutendaji kwa kuwa na Watumishi Wawili (2) tu, Mmoja (1) ni Afisa na mwingine ni Mlinzi ambao wapo katika Ofisi hiyo toka ilipoanzishwa katika Mwaka wa Fedha 2010/2011. Hivyo Ofisi hii inaendelea kuwa na changamoto nyingi za kiutendaji kutokana na upungufu wa Watendaji. Changamoto hii kwa kiasi kikubwa imeathiri sana utekelezaji wa majukumu ya Tume kwa upande wa Pemba.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutatua changamoto hiyo ya kiutendaji, Kamati imearifiwa kwamba, kutokana na ongezeko la fedha katika bajeti ya Tume katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Watumishi Wawili (2) wataongezwa katika Ofisi hiyo.

## 2.1 MAONI YA JUMLA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haijaridhishwa na kasi ya utoaji wa fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya

Maendeleo. Karibu miradi yote iliyotengewa fedha imepokea sehemu tu ya fedha iliyoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017. Vilevile Kamati inasikitishwa na hatua ya Serikali kutotoa fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Miradi mingi ya maendeleo imekuwa inategemea fedha za nje kwa kiasi kikubwa. Mfano, Wizara ya Katiba na Sheria **(Fungu 41)** ilipokea fedha za nje tu kwa ajili ya Mradi namba 6201 (E-Justice) kiasi cha Shilingi Bilioni Moja (**1,000,000.000.00**) na Mradi namba 6517 (Unicef Multi-Sectoral Support Program) ilipokea Shilingi Milioni Mia Tatu Tisini na Sita, Laki Nne Sabini na Mbili Elfu, Mia Sita Kumi na Tatu (**396,472,613.00**) zote zikiwa ni fedha za nje. Hapakuwa na fedha yoyote ya ndani iliyotolewa kwa ajili ya Miradi hii yote. Hali hii pia imejitokeza kwenye miradi mingine katika Taasisi zilizo chini ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** ili kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa fedha za ndani za kutosha kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo, uko umuhimu kwa kila Taasisi ya Serikali kubuni vyanzo vya mapato vitakavyosaidia kuongeza fedha za ndani ili kuepuka utegemezi wa fedha za nje.

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati ilikutana Mjini Dodoma Tarehe 31 Machi na 01

Aprili, 2017 kwa ajili ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara hii, Kamati ilizingatia mlinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge Mwezi Mei 2016 na kiwango ambacho kimepokelewa hadi kufikia Machi 2017.

**Mheshimiwa Spika**, lengo la kufanya tathmini ya namna hii ni kufahamu mwelekeo wa Mpango na Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 na kujua vipaumbele vya kibajeti katika Mwaka wa Fedha unaofuata.

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Wizara ya Katiba na Sheria kwa ujumla, ilidhiinishiwa Shilingi Bilioni Mia Moja Tisini na Moja, Milioni Mia Nne Hamsini, Laki Tisa na Moja (**191,450,900,001.00**) kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo Shilingi Bilioni Sitini na Tano, Milioni Mia Tisa Arobaini na Tisa, Laki Sita Arobaini na Tatu Elfu na Mia Tatu (**65,949,643,300.00**) ni kwa ajili ya Mishahara na Shilingi Bilioni Mia Moja na Nane, Milioni Mia Tano Sitini na Mbili, Tisini na Saba Elfu, Mia Tisa Sitini na Moja (**108,562,097,961.00**) ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Hadi kufikia Mwezi Disemba 2016, Wizara ilipokea jumla ya Shilingi Bilioni Tisini na Saba, Milioni Mia Mbili Hamsini na Tano, Laki Tano na Sita Elfu, Mia Mbili Thelathini na Tisa (**97,255,506,239.00**) sawa na asilimia 51 ya fedha

zilizoidhinishwa kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini.

**Jedwali Namba 1: Mlinganisho wa Fedha iliyotengwa na kupokelewa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 Chini ya Fungu 41 Hadi kufikia Disemba 2016**

| Fungu | Fedha Iliyoidhinishwa Sh. | Fedha Iliyopatikana Sh. | Tofauti Sh. | Asilimia Sh. |
|---|---|---|---|---|
| 41 | 191,450,900,001.00 | Sh.97,255,506,239.00 | Sh.94,195,393,762 | 51 |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatoa wito kwa Ofisi ya Hazina kutoa kiasi cha fedha kilichobaki ambacho kiliidhinishwa na Bunge kwa Wizara ya Katiba na Sheria katika kipindi hiki kilichobaki cha Mwaka wa Fedha 2016/2017 ili Wizara iweze kumaliza utekeleza majukumu yake kwa Ufanisi kama ilivyopanga.

| Fungu | Taasisi | Fedha Zilizoidhinishwa | Fedha Zilizopokelewa | Asilimia ya kiasi kilichopokelewa |
|---|---|---|---|---|
| 41 | Wizara ya Katiba na Sheria | Sh.9,141,681,000.00 | Sh.3,883,679,000.00 | 42 |
| 16 | Mwanasheria Mkuu wa Serikali | Sh.6,997,324,000.00 | Sh.5,306,378,890.89 | 76 |
| 35 | Mkurugenzi wa Mashtaka | Sh.13,097,619,000.00 | Sh.7,955,545,061.32 | 61 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 12 | Tume ya Utumishi wa Mahakama | Sh. 1,134,955,000.00 | Sh. 609,858,475.00 | 53.7 |
| 59 | Tume ya Kurekebisha Sheria | Sh. 1,658,192,000.00 | Sh.1,021,696,624.65 | 61 |
| 55 | Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | Sh. 3,741,929,226.22 | Sh.2,074,860,878.22 | 55.44 |

**Mheshimiwa Spika**, mchanganuo wa fedha zilizoidhinishwa na zilizopokelewa katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 hadi kufikia Machi 2017 katika Mafungu Sita yanayosimamiwa na Wizara hii, yaani Fungu 41, 16, 35, 59,55 na 12 umeainishwa kwenye jedwali hapa chini kwa kila Fungu.

**Jedwali Namba 2: Mlinganisho wa Fedha Iliyoidhinishwa na Kupokelewa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Hadi Kufikia Machi 2017**

**Mheshimiwa Spika,** katika mlinganisho ulioonyeshwa kwenye jedwali namba 2 hapo juu, Fungu 35 (Divisheni ya Mashitaka) ndio lililotengewa fedha nyingi zaidi ambazo ni Shilingi Bilioni Kumi na Tatu, Milioni Tisini na Saba, Laki Sita Kumi na Tisa Elfu (**13,097,619,000.00**) kwa Mwaka 2016/2017. Hata hivyo hadi kufikia Mwezi Machi, 2017 fungu hili limepokea Shilingi Bilioni Saba, Milioni Mia Tisa Hamsini na Tano, Laki Tano Arobaini na Tano Elfu Sitini na Moja (**7,955,545,061.00**).

**Mheshimiwa Spika**, katika mlinganisho huo, Tume ya Utumishi wa Mahakama **(Fungu 12),** liliidhinishiwa fedha kidogo zaidi kuliko mafungu mengine, kwa kiasi cha Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Moja Thelathini na Nne,

Laki Tisa Hamsini na Tano Elfu (**1,134,955,000.00**). Pamoja na kuidhinishiwa fedha hizo kidogo, hadi kufikia Mwezi Machi, 2017 fungu hili limepokea Shilingi Milioni Mia Sita na Tisa, Laki Nane Hamsini na Nane Elfu, Mia Nne Sabini na Tano (**609,858,475.00**).

**Mheshimiwa Spika**, mwenendo huu wa upokeaji fedha kwa ujumla, unadhihirisha kuwa, fedha inayopokelewa ni ndogo sana ukilinganisha na kiasi kinachoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Hivyo Taasisi hizi zinashindwa kutekeleza majukumu yake kwa wakati na ufanisi kutokana na ucheleweshaji wa utoaji wa fedha kwa upande wa Hazina**.**

## 3.1 UCHAMBUZI WA TAARIFA KUHUSU UKUSANYAJI MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake, ilitarajia kukusanya kiasi cha Shilingi Bilioni Kumi na Saba, Milioni Themanini na Tano, Laki Nane Ishirini na Tisa Elfu, Mia Tano Kumi na Moja (**17,085,829,511.00**) kama maduhuli ya Serikali kutoka vyanzo mbalimbali vya mapato. Hadi kufikia Mwezi Disemba, 2016, Wizara ilikuwa imekusanya kiasi cha Shilingi Bilioni Kumi, Milioni Mia Tisa Arobaini na Tatu, Laki Nne Tisini na Moja Elfu, Mia Nane Arobaini na Tano (**10,943,491,845.00**) sawa na asilimia 64 ya makusanyo yaliyotarajiwa kama ilivyochanganuliwa kwenye jedwali hapa chini

**Jedwali Namba 3: Mlinganisho wa Makadirio, Makusanyo na Asilimia Kwa Mafungu yaliyo Chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Hadi Kufikia Disemba 2016**

| Fungu | Makadirio | Makusanyo | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 12 | Sh. 0 | Sh. 0 | 0 |
| 16 | Sh. 3,002,000.00 | Sh. 0 | 0 |
| 35 | Sh.12,000,000.00 | Sh. 32,634,666.00 | 272 |
| 40 | Sh.6,504,130,428.00 | Sh.5,344,178,000 | 82 |
| 41 | Sh. 10,566,697,083 | Sh 5,599,313,845 | 53 |
| 55 | Sh.0 | Sh.0 | 0 |
| 59 | Sh.0 | Sh. 0 | 0 |
| Jumla | **Sh 17,085,829,511** | **Sh.10,943,491,845** | **64** |

**Mheshimiwa Spika**, makusanyo haya ni kutokana na ada mbalimbali za Usajili wa Matukio, Ada za Wanafunzi, Uuzaji wa Vitabu vya Zabuni na Huduma nyingine mbalimbali zinazotolewa na Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Katiba na Sheria **(Fungu 41)** imeongoza katika ukusanyaji wa Maduhuli kwa kukusanya Shillingi Bilioni Tano, Milioni Mia Tano Tisini na Tisa, Laki Tatu Kumi na Tatu Elfu, Mia Nane Arobaini na Tano (**5,599,313,845.00**) ikifuatiwa na Idara ya Mahakama **(Fungu 40)** iliyokusanya Shilingi Bilioni Tano, Milioni Mia Tatu Arobaini na Nne, Laki Moja Sabini na Nane Elfu (**5,344,178,000.00**).

**Mheshimiwa Spika**, mafungu mengine yalikuwa na matarajio ya kukusanya Maduhuli lakini matarajio hayakuwa kama yalivyopangwa. Hii ni changamoto ambayo Wizara na Taasisi zote zenye vyanzo vya mapato zinabidi kuiangalia kwa umakini kwani matarajio sio mapato. Hivyo kuna umuhimu wa kubuni vyanzo

vingine vya ukusanyaji wa Maduhuli ili kuongeza upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hasa kwa zile Taasisi zilizokosa mapato kabisa.

## 3.2 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uwasilishaji wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, Kamati ilitoa ushauri na mapendekezo Kumi na Sita (16) kuhusiana na Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefurahishwa na utekelezaji wa maoni ya Kamati yaliyotolewa katika Taarifa yake ya Uchambuzi wa Bajeti kwa Wizara hii Mwezi Mei, 2016. Jambo mahsusi ambalo Kamati imeridhika nalo, ni ongezeko kidogo kwenye Bajeti ya utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, ambayo imetengewa Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tano Sitini na Sita, Themanini Elfu (**1,566,080,000.00**) katika Mwaka ujao wa fedha (2017/2018) kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha uliopita ambapo Tume hii iliidhinishiwa Shilingi Milioni Mia Tisa Tisini na Nne, Laki Tano Kumi na Nne Elfu **(994,514,000.00)** tu kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ambayo ilikuwa ni ndogo na haikulingana na uzito wa majukumu yake katika kuhakikisha Haki za Binadamu na Utawala Bora zinazingatiwa. Tofauti hii ni ongezeko la asilimia 57 ya Bajeti inayoombwa kuidhinishwa kwa ajili ya Tume katika Mwaka wa Fedha unaokuja. Hata hivyo fedha iliyoidhinishwa haitoshelezi ikilinganishwa na

majukumu yanayopaswa kutekelezwa na Tume katika Nchi nzima. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuongeza fedha za kutosha kwa Tume hii ili itekeleze majukumu yake kikamilifu.

## 4.0 MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 Wizara ya Katiba na Sheria, imejiwekea malengo saba (7) ya kutekeleza ili kuongeza ufanisi na ubora katika kutoa huduma za Kisheria na masuala ya Katiba yakiwemo;

i) Kuendelea na uhamasishaji wa shughuli za Serikali kutoka Dar es Salaam kwenda Makao Makuu ya Nchi, Dodoma;
ii) Kuimarisha mfumo wa Sheria na kuongeza uwezo wa Wizara katika maeneo maalum ya Sheria, usimamizi na utoaji haki;
iii) Kuimarisha usimamizi na ufuatilaji wa masuala ya Kikatiba na Sheria;
iv) Kuimarisha misingi ya haki za Binadamu na Kisheria;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inakubaliana na malengo ya Wizara kwa ujumla kwani yanalenga katika kuboresha utekelezaji wa majukumu yake na kuleta ufanisi zaidi katika suala zima la utoaji haki nchini.

## 4.1 MAKADIRIO YA MAPATO YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara inatarajia kukusanya kiasi cha Shilingi Bilioni Ishirini na Nne, Milioni Themanini na Saba, Laki Tano na Saba Elfu, Mia Mbili (**24,087,507,200.00**) ikiwa ni Maduhuli ya Serikali, kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini:

**Jedwali Namba 4: Matarajio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

| **Fungu** | **Matarajio ya Maduhuli** |
|---|---|
| 12 | Sh. 0 |
| 16 | Sh. 3,002,000.00 |
| 35 | Sh. 13,002,000.00 |
| 40 | Sh. 9,318,061,200.00 |
| 41 | Sh. 14,753,292,000.00 |
| 55 | Sh. 0 |
| 59 | Sh. 150,000.00 |
| **Jumla** | **Sh. 24,087,507,200.00** |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa Makadirio ya Mapato hayaendani na hali halisi ya makusanyo. Hivyo

Kamati inashauri kuwa, ni vizuri kuweka makadirio madogo yenye uhakika katika kukusanya kuliko kuweka makadirio makubwa ya fedha ambayo hayana matarajio makubwa katika ukusanyaji.

**Mheshimiwa Spika,** Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora **(Fungu 55)** na Tume ya Utumishi wa Mahakama **(Fungu 12)** hayana matarajio yoyote ya kukusanya maduhuli kwa sababu ya kutokuwa na vyanzo vya mapato.

## 4.2 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara pamoja na Taasisi zake inaomba kuidhinishiwa **Shilingi Bilioni Mia Moja Hamsini na Tisa, Milioni Mia Tatu Thelathini na Moja, Laki Nane Ishirini na Mbili Elfu, (159,331,822,000.00)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo ambayo ni upungufu wa asilimia **4.4** ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/2017. Upungufu huu wa asilimia **4.4** unatokana na ukomo wa Bajeti ya fedha za maendeleo kupungua kwa wastani wa asilimia 55 ikilinganishwa na fedha ya Miradi ya maendeleo iliyoidhinishwa Mwaka 2016/2017.

**Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake, kwa Mwaka 2017/2018 inaomba fedha kama ilivoonyeshwa katika mchanganuo uliopo kwenye jedwali hapa chini.

**Jedwali Namba 5: Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

| Fungu | Taasisi | Kiasi |
|---|---|---|
| 41 | Wizara ya Katiba na Sheria | 9,862,066,000.00 |
| 16 | Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali | 7,282,523,000.00 |
| 35 | Divisheni ya Mashitaka | 14,914,063,000.00 |
| 12 | Tume ya Utumishi wa Mahakama | 1,102,911,000.00 |
| 59 | Tume ya Kurekebisha sheria | 2,052,757,000.00 |
| 55 | Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora | 6,166,981,000.00 |
| **JUMLA** | | **41,381,301,000.00** |

**Mheshimiwa Spika**, Divisheni ya Mashitaka **(Fungu 35)** lina makadirio ya matumizi ya juu zaidi ikilinganishwa na mafungu mengine. Bajeti inayoombwa kwa ajili ya Fungu hili ni sawa na asilimia **37%** ya Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, Tume ya Utumishi wa Mahakama **(Fungu 12)** lina Makadirio ya Matumizi madogo zaidi ikilinganishwa na mafungu mengine ikiwa ni sawa na asilimia 3.2% ya Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2017/2018.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia Taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati pamoja na majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zilizo chini yake, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao ili kuboresha utendaji kazi na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii.

i) Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza bajeti ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwa Fedha ya Matumizi Mengineyo (OC) kutoka **Shilingi Milioni Mia Tisa Tisini na Nne, Laki Tano Kumi na Nne Elfu** (**994,514,000.00**) katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 mpaka **Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tano Sitini na Sita, Themanini Elfu** (**1,566,080,000.00**) katika Mwaka wa Fedha ujao (2017/2018). Ongezeko hili ni sawa na asilimia **57.** Hata hivyo, Kamati inatoa rai kwa Wizara na Taasisi zake kufanya rejea ya maagizo yaliyotolewa na Kamati katika Taarifa ya Mwaka wa Fedha 2016/2017 na kuendelea kuyatekeleza katika kipindi cha robo ya mwisho ya mwaka huu wa Fedha unaoishia Mwezi Juni, 2017;

ii) Ofisi ya Hazina kutoa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa Wizara husika kwa wakati ili kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake kama yalivyopangwa katika kila Mwaka wa Fedha;

iii) Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria kufanya mapitio na maboresho yote ya msingi ya Sheria zote zinazohitaji maboresho na kutazama uwezekano wa kuhuisha Mchakato wa Upatikanaji wa Katiba Mpya kwa wakati muafaka;

iv) Wizara pamoja na Taasisi zake kukamilisha kwa haraka utekelezaji wa Mpango wa kuhamia Dodoma mapema iwezekanavyo ili kutekeleza uamuzi wa Serikali wa kuhamishia Makao Makuu ya Nchi Dodoma;

v) Kamati inatoa wito kwa Serikali kuleta Bungeni Sheria mahsusi ambayo itahalalisha utekelezaji wa maamuzi ya Serikali ya awamu ya Tano ya kuufanya Mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi;

vi) Tume ya Kurekebisha Sheria kuendelea kufanya mapitio ya Sheria mbalimbali kwa lengo la kuzirekebisha na kuziboresha ili kuendana na mabadiliko mbalimbali tuliyonayo sasa. Kamati inatoa rai kwa Tume hii kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ili kufanya mapitio ya Sheria ya Elimu ya Mwaka 1978 na kutazama uwezekano wa kuirekebisha ili kufanya Elimu ya Sekondari kuwa ya lazima na kuwawezesha vijana wanaomaliza Elimu ya Msingi kuendelea na Elimu ya Sekondari;

vii) Serikali kuongeza ukomo wa Bajeti kwa Wizara na Taasisi zake katika mwaka ujao wa fedha ili ziweze kuanza utaratibu wa kujenga majengo ya Ofisi zao katika mji wa Kiserikali utakaojengwa Dodoma;

viii) Wizara kuendelea kusimamia kwa ufanisi masuala yote ya haki za Binadamu na upatikanaji haki nchini na kuhakikisha kwamba inachukua hatua za kutosha kupunguza wingi wa kesi Mahakamani na wingi wa mahabusu katika rumande, jambo ambalo linavunja haki mbalimbali za watuhumiwa

ambao wanakaa rumande kwa muda mrefu bila kesi zinazowahusu kusikilizwa na kumalizika kwa wakati;

ix) Serikali kuzingatia kwa umakini matakwa ya Ibara ya 13(6) (a-e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 19777 ambayo inatoa haki za msingi za kuhusiana na watuhumiwa wa makosa ya Jinai ikijumuisha haki yakupata dhamana, kusikilizwa kwa kesi zao na kukata rufaa kwa wakati muafaka;

x) Wizara na Mhimili wa Mahakama kwa ujumla, kuzingatia matakwa ya kisheria kuhusu uendeshaji wa kesi za jinai na hususani taratibu za utoaji wa dhamana kwa watuhumiwa kama zilivyowekwa na kifungu cha 148 cha Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Jinai iliyopitiwa Mwaka 2002 (*Criminal Procedure Act* ). Kamati inasisitiza kwamba dhamana ni haki ya Mtuhumiwa na ni suala la Kikatiba. Hivyo Taasisi za utoaji haki zinapaswa kuzingatia suala hili ili kutenda haki kwa watuhumiwa;

xi) Serikali kuridhia na kutekeleza Mikataba mbalimbali ya Kimataifa iliyoridhiwa na Nchi yetu ili iweze kutekelezwa kama vile Mkataba wa Kimataifa wa Mwaka 1984 unaopinga matendo yote ya kikatili dhidi ya mwanadamu (*Convention Against Torture*, 1984);

xii) Wakala wa Usajili,Ufilisi na Udhamini (RITA) kuendelea kufanya kazi kwa kuzingatia misingi ya Sheria, Taratibu, Kanuni, uadilifu na weledi katika usajili wa mabaraza ya wadhamini wa vyama vya siasa au makundi mengine ya kijamii kwa

kusimamia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo, hivyo kuepuka kuwa sehemu ya migogoro ya vyama hivyo;

xiii) Wizara kuanzisha na kukamilisha mchakato wa upatikanaji wa Kanuni za Sheria ya Utoaji wa Msaada wa Kisheria ( *The Legal Aid Act* ) iliyopitishwa na Bunge katika Mkutano wa Sita wa Bunge uliofanyika Mwezi Februari, 2017;

xiv) Tume ya Utumishi wa Mahakama kusimamia kwa umakini mkubwa maslahi ya Mahakimu wote na hasa upandishaji wa vyeo na nyongeza ya mishahara kwa mahakimu walioko kwenye Mahakama za Mwanzo. Kamati inafahamu kwamba wapo mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ambao hawajapandishwa vyeo kwa miaka zaidi ya Saba (7) kinyume kabisa na taratibu za kazi na ajira kwa Watumishi wa Umma;

xv) Kamati inatoa wito kwa Watendaji wa Mahakama wa Wilaya kufanya kazi kwa weledi na kwa kuzingatia Sheria,Taratibu na Mipaka ya Kazi zao na kutokuingilia majukumu ya msingi ya Mahakama katika kutoa na Kusimamia Haki;

xvi) Wizara na Mhimili wa Mahakama **(Fungu 40)** kuendelea kuboresha mfumo wa utoaji haki nchini na uendeshaji wa kesi kwa kutumia njia na mifumo ya Kisasa ya Mawasiliano (E-Justice). Kamati inawapongeza wadau wote wa Maendeleo kama Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na Shirika la Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) ambayo yamekuwa mstari wa mbele katika kufadhili Miradi mbalimbali ya

Maendeleo iliyo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria ukiwamo mradi huu wa E-Justice.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, mwisho napenda kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii muhimu kuwasilisha maoni ya Kamati yangu. Aidha, hatuna budi kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa busara, umakini na umahiri mkubwa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Dr. Harrison G.Mwakyembe aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria, ambaye kwa zaidi ya mwaka mmoja alifanya kazi kwa weledi na kutoa ushirikiano mkubwa kwa Kamati wakati wa utekelezaji wa majukumu yake, hasa katika wakati

wa uchambuzi wa Sheria ya Huduma za Utoaji wa Msaada wa Kisheria ya Mwaka 2016.

**Mheshimiwa Spika**, napenda nitumie nafasi hii pia kumshukuru Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb), Katibu Mkuu Prof. Sifuni Ernest Mchome, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Amon Mpanju na Watendaji wote wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa ushirikiano mkubwa walioutoa wakati Kamati ilipojadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya wakati wa kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Uzalendo, uchapakazi pamoja na ushirikiano mkubwa walionipa umesaidia kufanikisha kukamilika kwa Taarifa hii kwa wakati. Kwa ruhusa yako naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama yalivyo yaani Hansard.

(i) Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa, Mb, **Mwenyekiti**

(ii) Mhe. Najma Mutraza Giga, Mb, **Makamu Mwenyekiti**

(iii) Mhe. Ajali Rashid Akbar, Mb, Mjumbe

(iv) Mhe. Ally Saleh Ally, Mb, Mjumbe

(v) Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb, Mjumbe

(vi) Mhe. Asha Abdallah Juma, Mb, Mjumbe

(vii) Mhe. Dkt Mathayo David Mathayo, Mb, Mjumbe

(viii) Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb, Mjumbe

(ix) Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb, Mjumbe

(x) Mhe. Joseph Kizito Mhagama, Mb, Mjumbe

(xi) Mhe. Juma Hamadi Kombo,Mb,Mjumbe

(xii) Mhe. Makame Mashaka Foum, Mb, Mjumbe

(xiii) Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb, Mjumbe

(xiv) Mhe. Nassor Suleiman Omar, Mb, Mjumbe

(xv) Mhe. Omary Ahmed Badwel, Mb, Mjumbe

(xvi) Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb, Mjumbe

(xvii) Mhe. Riziki Shahari Mngwali, Mb, Mjumbe

(xviii) Mhe. Saumu Heri Sakala, Mb, Mjumbe

(xix) Mhe. Seif Ungando Ally, Mb, Mjumbe

(xx) Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb, Mjumbe

(xxi) Mhe. Suleiman Masoud Nchambi, Mb, Mjumbe

(xxii) Mhe. Taska Restituta Mbogo, Mb, Mjumbe

(xxiii) Mhe. Twahir Awesu Mohamed, Mb, Mjumbe

(xxiv) Mhe. Wanou Hafidhi Ameir, Mb, Mjumbe

(xxv) Ussi Pondeza, Mb, Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, vilevile napenda kuwashukuru kwa dhati, Watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge, kwa kusaidia na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Kipekee, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya

Kamati za Bunge Ndugu Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi, Ndugu Angelina Sanga na Makatibu wa Kamati Ndugu Stella Bwimbo na Ndugu Dunford Mpelumbe pamoja na Msaidizi wa Kamati, Ndugu Raheli Masima, Makatibu Muhtasi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Chiku Ramadhan, Ndg. Grace Wambura na Ndg. Irene Makongoro kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono Hoja.

Mohamed Omary Mchengerwa, Mb.

**MWENYEKITI,**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA NA SHERIA**

25 Aprili, 2017